



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HJD/L.40/9/99

21/02/ 2022

**TANGAZO LA AJIRA YA MUDA MFUPI LA KAZI YA KUKUSANYA
TAARIFA ZA MFUMO WA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwatangazia **nafasi 100 (mia moja)** za ajira ya muda ya kazi ya kukusanya taarifa za Postikodi na kuingiza katika Mfumo wa Anwani za Makazi kwa Kata na Mitaa yote ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Zoezi hilo linatarajia kufanyika kwa muda wa **siku 45** ikiwa ni kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kusajili taarifa za Anwani na Makazi katika Mfumo huo ifikapo Mwezi Mei, 2022.

A. SIFA ZA WAOMBAJI

Mwombaji awe na sifa zifuatazo;

- a) Awe raia wa Tanzania na anayeishi katika Jiji la Dodoma
- b) Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi 40
- c) Awe na kitambulisho au namba ya NIDA
- d) Awe na simu janja ya aina ya Android yenye uwezo wa kutunza chaji kwa siku nzima na aweze kuitumia
- e) Awe na barua pepe (e-mail address) na nywila (Password) inavofanya kazi
- f) Awe na uwezo wa kusoma Ramani za Mitaa

B. KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kutoa / kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- (ii) Kukusanya na kuingiza taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma pamoja na wamiliki wake kwenye mfumo wa Anwani za Makazi
- (iii) Kutuma taarifa (Data) kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi

C. MALIPO

Kazi itafanyika kwa muda wa **siku 45** kuanzia mwezi Machi 2022 kwa malipo ya **Tsh.30,000/=** kwa siku

D. MAOMBI YA AMBATANISHWE NA:


- (i) Nakala ya **Cheti cha Kidato cha Nne** na kuendelea
- (ii) Nakala ya **Cheti cha Kuzaliwa**
- (iii) Nakala ya **Kitambulisho cha NIDA** (kama anacho) au aainishe **Namba ya NIDA**
- (iv) **Picha 2** za hivi karibuni (Current Passport Size)

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI YA KAZI

1. Barua zote za maombi ya kazi zitumwe kwa;

MKURUGENZI WA JIJI,
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA,
S. L. P 1249,
DODOMA

2. Barua zote za maombi ya kazi zipitishwe na Mtendaji wa Mtaa na Kata anayoishi mwombaji.
3. Upande wa mbele wa Bahasha ya Maombi, eneo la juu kulia iandikwe; **Kumb. Na. HJD/L.40/9/99**
4. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Jumatano tarehe **23 Februari 2022**, Muda wa saa **9:30 Alasili**.


Joseph C. Mafuru
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji,
DODOMA.

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S. L. P. 1249,
DODOMA